Haki Itokeayo Ndani Kuja Nje

Sura ya 15

Somo la Kusikiza: Agano Jipya 15

Shabaha: Kuchunguza mafundisho ya Yesu katika mazungumzo yake na watu wengine.

Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe,ajitwike msalaba wake, anifuate. Kwa maana mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona. Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?

- Mathayo 16: 24-26

Yesu alitangaza kuwa atajenga kanisa lake, na malango ya kuzimu hayatamzuilia. Mazingara ya tangazo hili ni kuwa Yesu aliwauliza mitume wake, "Nanyi mwasema kuwa mimi ni nani?" Petero akajibu, "Wewe ni Kristo!" ambalo linamaanisha Masihi aliyeahidiwa.

Kama kulivyo muhimu kukiri huku kwa Petero, jibu la Yesu kwa kukiri huku ni muhimu hata zaidi. Yesu alikuwa wazi kuwa Petero hakujibunia jibu hilo. Baba alikuwa amemfunulia. Yesu angejenga kanisa lake juu ya muujiza huu kwamba mtu wa kawaida kama Petero angesema jambo la ajabu kama hilo. Kwa hakika kanisa litajawa na watu wa kawaida wanaofanya mambo yasiyo ya kawaida, kwa sababu wametiwa nguvu kwa Roho Mtakatifu.

Ni muhimu kwetu pia kuwa na jibu sahihi kwa swali hili ambalo Yesu aliwauliza mitume. Tunapaswa kujua kuwa yeye ni Yesu ambaye ni Kristo, aliye Masihi, Mkombozi tuliyeahidiwa na Mwokozi wa ulimwengu.

1. Ukwli au **uongo**? Wanafunzi walipomwona Yesu akitembea juu ya maji, mara walijazwa imani na ujasiri.

2. **Ukweli** au uongo? Petero hakutembea juu ya maji hadi alipokuwa na hakika kuwa Bwana anamwita.

3. **Ukweli** au uongo? Yesu alingojea hadi Petero alipomwita, hadi alipoomba kabla ya kumjia na kumwokoa.

4. **Ukweli** au uongo? Yesu alifundisha kwa njia zingine nyingi kando na mifano.



5. Ukweli au **uongo**? Mazungumzo ya Yesu na wakuu wa dini kila mara yalikuwa ya upole na ya kirafiki.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

6. Ni gani kati ya maneno yafuatayo linaloelezea wanafunzi juu ya chombo katikati ya dhoruba?
   a. Waliojawa na imani
   b. Waliochangamka
   c. **Walioshituka**
   d. Waliotiwa pumzi na Mungu

7. Ni gani kati ya maneno yafuatayo linaloelezea haki ya Mafarisayo?
   a. Safi
   b. **Ya nje**
   c. Ya ndani
   d. Iliyotiwa pumzi na Mungu

8. Yesu alisema nini kuhusu mapokeo ya viongozi wa kidini?
   a. Hayakutokana na maandiko
   b. Yalipatikana kwa maandiko
   c. Yalikuwa bora kuliko maandiko
   d. Kila mara yalikuwa ya kuelekeza na ya msaada

9. Mapokeo ya utamaduni yanatumika vipi kwa Wakristo wa leo?
   a. Hatuna mapokeo ya utamaduni leo. Sisi tunatenda tu yalioyoandikwa
   b. Utamaduni kila mara ni mbaya na wa dhambi
   c. Utamaduni unaweza kuwa wa muhimu wakati mwingine, lakini hauwezi kujukuliwa kuwa wa muhimu kama maandiko
   d. Utamaduni ni kitu cha kiungu – ishara ya Mungu kuendelea kujifunua kwa wanadamu

10. Nini hufanya wanadamu kuwa wafisadi?
    a. Hali za bahati mbaya
    b. Msukumo kutoka kwa watu wengine
    c. Umasikini
    d. Asili ya dhambi ndani yetu

11. Jibu la Petero lilikuwa nini kwa swali la Yesu, “Nanyi mnasema mimi ni nani?”
    a. Mwalimu mkuu
    b. Nafsi iliyotiwa nuru
    c. Kristo Mwana wa Mungu
    d. Eliya ambaye amezaliwa tena

12. Nani aliyemfunulia Petero Yesu ni nani?
    a. Mungu Baba
    b. Mmoja wa wanafunzi wengine
    c. Hekima ya Petero mwenyewe
    d. Hakuna. Alijaribu tu na akapata jibu sahihi

Kama Yesu angekuuliza wewe unadhani Yeye ni nani, ungemjibu vipi? Ni kwa njia gani amejifunua mwenyewe kwako? Je, unakumbana na dhoruba zozote maishani mwako? Yesu anataka wewe uitikie vipi?

_____

_____

_____

Shukuru Mungu kwamba analojibu kwa shida yetu ya dhambi na kuwa Yesu hututakasa kutokea ndani kuja nje. Mshukuru Mungu kuwa kila mara anaahidi kuwa pamoja nasi hata katikati ya dhoruba. Muulize aendelea kusafisha moyo wako ili umtumainie zaidi.

KUZAMA ZAIDI

1. Fafanua namna utofauti kati ya haki aliyofundisha Yesu na haki ya Mafarisayo ulivyokuwa wa ndani na si wa nje, wa wima na si wa mlazo, na wa kimaandiko na si wa kitamaduni. _____
_____
_____
_____

2. Tunatumiaje mafundisho ya Yesu (kama yalivyonakiliwa katika Mathayo 15) kuwa mambo yanayo sababisha tutende dhambi si ya nje-ndani, kama mazingara, lakini ni ya ndani-nje, au mambo ya moyo? _____
_____
_____

3. Ni yapi yaliyo matumizi kwa mazingara haya ya mkazo wa tangazo la Yesu kuwa mamlaka ya Imani na matendo yaliyo nje ya Biblia, hayapaswi kuwekwa kwa nafasi ya mamlaka kamili ya imani na matendo tunayopata katika Neno la Mungu lililotiwa pumzi? (Fikiria juu ya wale kama Mormons, Wanasayansi Wakristo, na wengineo ambao wana mamlaka ya imani na matendo yatokayo nje ya Biblia.) _____
_____

4. Tunawezaje kutumia mafundisho ya Yesu kuwa tunapaswa kujikana wenyewe, tujukue msalaba wetu na kumfuata, na kisha tupoteze maisha yetu ili tuyapate? _____
_____
_____

5. Ni nini kinachopaswa kuwa matumizi yetu ya binafsi ya mafundisho ya Yesu katika mazungumzo yake na Petero kuhusu nani aliyemfunulia jibu kwa swali, *"Ninyi mnasema mimi ni nani?"* _____
_____
_____

6. Ni ukweli gani tunaoweza tumia kwa uhalisi kuwa Petero hakutembea juu ya maji hadi alipokuwa na hakika kuwa ni Bwana na kuwa Bwana wake alikuwa amemwalika atembee juu ya maji? _____
_____
_____

7. Vile ilivyonakiliwa katika Mathayo 16:24-26, ni thamani gani ambayo Bwana aliweka juu ya nafsi zetu na alimaanisha nini kwa kusema nafsi zetu? _____
_____
_____